ACT
Agricultural Council of Tanzania

Tunaunganisha, Shawishi Na Kutetea

TOLEO Na.46 (APRILI-JUNI 2023)



# JARIDA LA ACT 2023

## Yaliyomo


- Kongamano la TIsa la Wadau Wa Sekta ya Kilimo
- Warsha ya Uongozi
- Warsha ya Kikanda - Usimamizi wa Maarifa
- Programu ya Kuwajengea Uwezo Vijana
- Misheni Mashambani
- Kikao Cha Wadau - CARE Tanzania na SUA
- Warsha ya Kikanda - Mabadiliko ya Tabianchi
- Mafunzo - Mbinu Bora za Kilimo
- Wakulima na Wauza Pembejeo Wajadili


## Tukio Lijalo

Agosti 1 - 8, 2023 - Maonesho ya Nane Nane Mbeya katika Viwanja vya John Mwakangali

Septemba 5 - 8, 2023 - Kongamano la Mifumo ya Chakula, JNICC Dar es Salaam – Tanzania

Agosti 10 - 12, 2023 - Maonesho ya Kimataifa ya Bidhaa za Kilimo, Diamond Jubilee Hall- Dar es Salaam

Oktoba 11 - 13, 2023 - Maonesho ya Kimataifa ya Korosho, JNICC- Da res Salaam

Oktoba 13 & 14, 2023 -Maonesho ya Ndege wa Fugwao, Dar es Salaam- Ubungo Plaza

## Habari Muhimu



### Jarida la 2

Warsha ya Uongozi

Taasisi ya African Agribusiness Academy (AAA) iliendesha mafunzo ya siku nne yenye yaliyohusu Uongozi na Ubunifu kwa taasisi mwamvuli za kilimo. Mafunzo hayo yaliendeshwa kuanzia Mei 15 mpaka 18, 2023 jijini Arusha katika Hoteli ya Gold Crest, kupitia mradi wa BFC.



### Jarida la 3

Warsha ya Kikanda

Shirika la Pan African Farmers Organization (PAFO), kwa kushirikiana na washirika wake, waliandaa Warsha ya Kikanda kuhusu usimamizi wa maarifa katika utekelezaji wa mradi wa FO4ACP.

# KONGAMANO LA TISA LA WADAU WA SEKTA YA KILIMO

Aprili 13 na 14 2023, Jukwaa la Wachambuzi na Watafiti wa Sera (Policy Analysis Group- PAG) waliandaa Kongamano la tisa (9) la Mwaka la Kisera (Annual Agricultural Policy Conference) lililofanyika Dodoma Hotel jijini Dodoma. Kongamano la mwaka huu, lilipambwa na kaulimbiu isemayo ***"Tanzania shindani kwenye Biashara Huru Barani Afrika (AfCFTA): Changamoto na Fursa kwenye Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi,"*** Kongamano hilo, lilihudhuriwa na wadau takribani 200 wakiwemo wabia wa maendeleo, watunga sera kutoka sekta za kilimo, usalama wa chakula, na lishe, watafiti, wasomi, wakulima, wafugaji na wavuvi na wanawake.

Kongamano hilo lilitumika kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera kupitia Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Afrika (CAADP) kwa kuangazia zaidi eneo la Usalama wa Chakula na Lishe. Pia wadau walijadili kuhusu mafanikio, mafunzo muhimu yaliyopatikana, mapungufu yaliyopo ambayo yanahitaji utatuzi, na mbinu za kimkakati za kuimarisha ushindani ndani ya muungano.

Halikadhalika wadau walijadili utayari wa Tanzania kutumia Jukwaa huru la biashara barani Afrika (AfCFTA), kufikia masoko kwa lengo la kutangaza na kuuza bidhaa zao. ACT iliwakilishwa na Mwenyekiti wake, Dkt. Jacqueline Mkindi, ambaye aliwasilisha mada iiliyoangazia fursa zilizopo kwa wafanyabiashara katika eneo huru la biashara barani Afrika (AfCFTA). Aidha, alisisitiza wafanyabiashara kutoka Tanzania kuchangamkia masoko mapya kupitia AfCFTA na kuzalisha kulingana na uhitaji.

Kongamno hilo la kila mwaka huandaliwa na kikundi cha Uchambuzi na Utafiti wa Sera (Policy Analysis Group – PAG) kwa kushirikiana na sekta zinazohusiana na kilimo na taasisi zingine 15, zikiwemo taaisis zisizo za kiserikali, taasisi za elimu ya juu, na sekta binafsi. Kongamano la 9 (AAPC) bila shaka limeacha alama, kwa kutoa mitazamo mipya, na mbinu za kuendeleza sekta ya kilimo kuelekea ushindani katika eneo huru la biashara barani Afrika (AfCFTA).



# WARSHA YA UONGOZI

Taasisi ya African Agribusiness Academy (AAA) iliendesha mafunzo ya siku nne yenye yaliyohusu Uongozi na Ubunifu kwa taasisi mwamvuli za kilimo. Mafunzo hayo yaliendeshwa kuanzia Mei 15 mpaka 18, 2023 jijini Arusha katika Hoteli ya Gold Crest, kupitia mradi wa Beyond Farming Collective (BFC). Mafunzo hayo yaliwaleta pamoja washiriki kutoka Mashirika mashuhuri ya Sekta ya Chakula cha Kilimo kama vile TAHA, ANSAF, SUGECCO, TFC, TAMPA, na TAWFA n.k..

Mafunzo yalilenga kuhamasisha na kuwawezesha viongozi na wasimamizi wa vyama mwamvuli kwenye sekta ya kilimo (member based) vinavyowakilisha wazalishaji, wasindikaji na wafanyabiashara kwa kuwaongezea maarifa yanayohitajika katika ungozi wa taasisi zinazoundwa kwa mfumo wa uanachama. Mafunzo yalijikita katika ukuzaji na uimarishaji wa biashara bunifu na endelevu, na kutoa huduma zinazokidhi matakwa ya wanachama (membership needs). Mafunzo yaliendeshwa na wataalam kutoka Taasisi ya KT Royal Tropical, kwa ushirikiano na Bopinc kutoka Nairobi

ACT iliwakilishwa na Bi. Laetitia William, Bw. Khalid Ngassa, na Bw. Dionis Kawanara ambao walibuni wazo la kutoa huduma kwa wanachama kwa lengo la kushughulikia changamoto za masoko.

## WARSHA YA KIKANDA - USIMAMIZI WA MAARIFA

Shirika la Pan African Farmers Organization (PAFO), kwa kushirikiana na washirika wake, waliandaa Warsha ya Kikanda kuhusu usimamizi wa maarifa katika utekelezaji wa mradi wa FO4ACP. Warsha hiyo ilifanyika kuanzia Mei 16 hadi 18 2023 katika Hoteli ya Lemigo-Kigali Rwanda. Mkutano huo, ulipambwa na kaulimbiu isemayo ***"Kujifunza Maarifa Yanayotufanya Tuwe Imara Zaidi"*** na uliwakutanisha wawakilishi wa Mashirika ya wakulima kutoka mabara tofauti (Afrika, Caribbean na Pacific) ambao ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa FO4ACP.

Warsha hii ya kimataifa, iliandaliwa na shirika la PAFO kwa lengo la kubadilishana maarifa, kujadili changamoto na kuboresha namna ya kutekeleza mradi wa FO4ACP. Rais wa PAFO Bw. Kolyang Palebele katika hotuba ya ufunguzi alisisititiza kazi kubwa iliyopo (utekelezaji wa Mradi), licha ya mafanikio makubwa yaliyopatikana hadi sasa. Washiriki pia walitumia nafasi hiyo kufanya tathmini ya utekelezaji wa mradi wa FO4ACP (MTR) kwa pamoja, kutathmini kazi iliyopo, mikakati ya kuboresha na kuhakikisha mafanikio ya mradi yanakuwa ya muda mrafu na endelevu.

ACT iliwakilishwa na, Bw. Obed Abraham (Msimamizi wa Mradi), ambaye alibadilishana maarifa kwa kuonesha ni namna gani Baraza la Kilimo linatekeleza mradi wa FO4ACP katika wilaya ya Mvomero. Ushirikiano huu umewezekana kupitia ufadhili kutoka Umoja wa Ulaya (EU), Umoja wa Nchi za Afrika, Caribbean na Pasifiki (OACPS), na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD), kupitia Shirikisho la Vyama vya Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU). Warsha ya Kikanda kupitia mradi wa FO4ACP ilitumika kama jukwaa muhimu katika kupashana maarifa na kuboresha mashirikiano baian ya Mashirika ya wakulima kutoka mataifa mbalimbali.





# PROGRAMU YA KUWAJENGEA UWEZO VIJANA

Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) kwa kushirikiana na Andreas Hermes Akademie (AHA- International) walihitimisha kwa mafanikio ***"Programu ya Kuwajengea Uwezo Vijana"*** kwa nchi wanachama wa SADC. Aprili 25 mpaka Mei 1, 2023 SACAU waliendesha warsha ya kuhitimisha mafunzo huku wakilenga zaidi kubadilishana uzoefu na kuainisha fursa zilizopo katika sekta ya kilimo. Mbali na mafunzo, SACAU waliendesha Mkutano wa Kisera wa Mwaka (Annual Policy Conference 2023) uliofanyika Polokwane. Warsha ya Mwaka ya Sera ilikutanisha wanachama 19 wa SACAU kutoka nchi 12. Lengo kuu la warsha hiyo lilenga kujadili mabadiliko ya tabianchi na namna gani Mashirika ya Wakulima (NFOs) yanaweza kuwa sehemu ya kutekeleza mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Sambamba na warsha hii, washiriki wa Mkutano wa Sera na watahiniwa wa Programu ya Kujengewa Uwezo walipata fursa ya kufanya ziara ya mafunzo katika mashamba makubwa ya kilimo ambayo ni ZZ2 na Marlo. Ziara hiyo, iliwawezesha kujifunza mbinu bora za kilimo cha mboga mboga, tufaha, maua ya waridi, na ufugaji wa ng'ombe wa nyama.





Katika hotuba ya kufunga Rais wa SACAU Dkt. Sinare Y. Sinare aliwahimiza wahitimu kutumia ujuzi waliopata kupitia program ya vijana kuimarisha biashara zao na kuleta matokeo chanya katika shughuli zao. ACT iliwakilishwa na Bw. Jitu Soni (Makamu Mwenyekiti) na Bw. Timoth Mmbaga (Mkurugenzi Mtendaji)



# MISHENI MASHAMBANI

Kuanzia Juni 25 hadi Julai 4, 2023, ACT iliendesha ziara ya kikazi katika wilaya tisa ambazo ni: Handeni, Kilindi, Kondoa, Babati, Monduli, Meru, Hai, Siha na Moshi Vijijini. Ziara hii ililenga kuongeza uelewa wa kina kwa wakulima wadogo kuhusu bidhaa zinazozalishwa na kampuni ya BAYER (Mbegu na Madawa). Zoezi hilo liliendeshwa na Bw. Khalid Ngassa, Bw. Obed Abraham na Bi. Susan Masagasi, ambao walikuwa na jukumu la kuwaelekeza wakulima kanuni na miongozo ya Kilimo Bora (GAP) na kuchambua fursa za masoko kwa bidhaa wanazozalisha.

Ziara hiyo ilikuwa na malengo makuu mawili; kufanya ukaguzi wa mashamba darasa na kuweka mabango yanayoonyesha aina ya mbegu iliyopandwa ili kuonyesha utofauti kati ya bidhaa za BAYER na kampuni nyinginezo. Kupitia mkakati wa mashamba darasa, wakulima walitoa michango yao kwa kuelezea ufanisi wa bidhaa za BAYER na kuonyesha uhitaji mkubwa wa bidhaa hii katika shughuli za kilimo.

Ushirikiano huu kati ya ACT na BAYER, ulilenga kuongeza tija na hamasa kwenye kilimo cha mahindi kupitia matumizi ya mbegu za DK—kutokana na ufanisi wake. Timu kutoka Sekretarieti ilivutiwa na matokeo chanya ya mbegu za DK katika wilaya zilizo ndani ya mradi. Aidha, wakulima walionyesha kuridhishwa na utendaji kazi wa bidhaa za BAYER kutokana na wingi wa mavuno.




Kimsingi, ziara ya kikazi ilikuwa sehemu muhimu kutathmini ufanisi wa mashamba darasa, kutoa miongzo kwa wakulima viongozi na utambuzi wa fursa za masoko. ACT ilihakikisha mashirikiano kati wakulima na wadau kwenye mnyororo wa thamani wa zao la mahindi yanaboreka na wanakuwa sehemu ya utekelezaji wa mradi

Ufanisi katika utekelezaji wa mradi huu, unaonyesha dhamira ya ACT kuwawezesha wakulima wadogo na kuhimiza matumizi ya mbegu bora kwa kilimo endelevu. Kupitia ushirikiano huu, ACT inalenga kuleta mabadiliko chanya katika kuendeleza sekta ya kilimo.



# KIKAO CHA WADAU - CARE TANZANIA NA SUA

Juni 6 na 7, 2023 Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) na shirika la CARE Tanzania waliendesha warsha ya pamoja iliyofanyika katika Hoteli ya Nashera jijini Dodoma. Warsha hiyo iliwakutanisha wadau kutoka taasisi za umma na binafsi ambazo ni; ACT, ANSAF, SAGCOT, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, pamoja na wawakilishi kutoka Halmashauri ya Iringa na Arusha ambako mradi wa Scale Up unatekelezwa.

Lengo kuu la mkutano wa wadau ilikuwa kufanya mapitio ya kina ya mitaala ya programu zinazotolewa (shahada) katika chou kikuu cha Sokoine (SUA). Mapitio ya shahada hizo yalijumuisha; Shahada ya Sayansi ya Kilimo (BSc. CD), Shahada ya Sayansi ya Maendeleo ya Jamii (BSc. CD), Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Maendeleo ya Jamii (MSc. CD), Shahada ya Uzamili ya Ugani, Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Mawasiliano na Uandishi wa Habari ( MSc.ACJ) n.k

Dkt. Rasel Madaha kutoka SUA na Bi.Christina kutoka CARE Tanzania waliongoza warsha kwa kuelezea jinsi CARE na SUA walivyokusudia kuboresha mitaala kwa lengo la kuzalisha watahiniwa wanaokidhi hitaji la soko. Bi.Christina alielezea mradi unaotekelezwa na CARE Tanzania (SCALE UP) katika vijiji 62 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, ukilenga kuongeza tija kwenye mnyororo wa thamani wa mazao ya alizeti na soya.

Warsha hii ilitumika kama jukwaa la kukusanya maoni ya wadau kuhusu ubora wa programu zitolewazo na kuainisha maeneo ya kuboresha. Mapendekezo yaliangazia zaidi wingi kozi, baadhi ya kozi kuunganishwa pamoja, kutoa kipaumbele katika ujuzi kwa vitendo na kuunganisha mtaala wa masomo ujulikanao kama FFBS (Farmer Field Busines School)  katika program za somo SUA.

Ushirikiano kati ya SUA, CARE Tanzania, na wadau wengine ni chachu ya kuleta mabadiliko katika elimu ya ngazi ya juu hususani program za kilimo. ACT iliwakilishwa na Bw. Khalid Ngassa ambaye alitoa mchango kuhusu aina ya ujuzi ambao mashirika ya  kilimo yanahitaji kutoka kwa wahitimu wa program za elimu ya juu.



# WARSHA YA KIKANDA – MABADILIKO YA TABIANCHI

Juni 22 na 23, 2023 Shirikisho la Wakulima Kusini Mwa Afrika (SACAU) liliandaa warsha ya Kikanda kuhusu mabadiliko ya tabianchi iliyofanyika katika hoteli ya Birchwood jijini Johannesburg, Afrika ya Kusini. Warsha hiyo iliwakutanisha washiriki 87 kutoka nchi 12 ambazo ni wanachama wa SACAU. Mtendaji Mkuu wa SACAU Bw. Ishmael Sunga alisisitiza umuhimu wa kuongeza ushirikiano baina ya Serikali, Azaki za Kiraia, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Vyama Mwamvuli vya Kilimo katika kutoa elimu na kutekeleza mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Warsha ya Kikanda ililenga kuhamasisha wanachama wa SACAU kuhusu umuhimu wa kushughulikia vipaumbele vya nchi katika kukabiliana na masuala ya mabadiliko ya tabia ya nchi kwa mustakabali wa ustawi wa sekta ya kilimo. Pia, warsha ililenga kuainisha maeneo muhimu ya kufanyia kazi baina ya vyama mwamvuli na Serikali katika kutekeleza mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Washiriki walipata fursa ya kupokea mrejesho wa tafiti zilizofanyika nchi nane (8) kuhusu ***"Kupima Uwezo wa Vyama vya Wakulima katika Kutekeleza Mpango Mkakati na Sera za Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika Ngazi ya Kitaifa."*** Bw. Bertus Kruger, mtaalamu elekezi kutoka Namibia katika wasilisho lake alijaribu kugusia fursa za mashirikiano zilizopo katika kutekeleza mpango wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuwasaidia wakulima kukabliana na changamoto zinazohusiana na tabianchi. ACT iliwakilishwa na Bw. Jitu Soni (Makamu Mwenyekiti), Bw. Khalid Ngassa (Meneja Uanchama) na Bi. Avelina Bernard (Afisa Sera) ambao kwa pamoja walitoa taswira ya nchi katika kutekeleza mpango wa kukabiana na mabadiliko ya tabia ya nchi. Warsha ya Kikanda ilionekana ni jukwaa muhimu sana katika kubadilishana uzoefu na kuanisha maeneo ya kimkakati ya kufanyia kazi katika kukabilana na mabadiliko ya tabianchi.

# MAFUNZO - MBINU BORA ZA KILIMO

Mei 03 hadi 06 2023, Afisa Mradi kutoka ACT Bw. Obedi Abraham na Meneja Uanachama Bw. Khalid Ngassa waliendesha mafunzo ya siku nne kuhusu ***"Mbinu Bora za Kilimo na Matumizi Sahihi ya Pembejeo kwa Kilimo Shadidi Kwenye Zao la Mpunga (SRI)"*** kwa wakulima wa Wilaya ya Mvomero-Mkoani Morogoro katika skimu za umwagiliaji,- Mkindo na Dakawa. Mafunzo yalilenga kuwajengea uwezo wakulima kwa kuwapa mbinu bora za kilimo hasa kilimo shadidi ambacho kwa kiasi kikubwa hakitegemei mvua, na mbinu bora za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Jumla ya washiriki 62 (Wakulima viongozi - kina mama 31, vijana 17 na Maafisa ugani 6) walipatiwa mafunzo. Mafunzo yalikusudia kufundisha wakulima viongzo 25 ambao watawafikia wakulima wengine kwa mafunzo na kufanya idadi iwe 1500. Pia, mafunzo yalitumika kama jukwaa muhimu kwa wakulima kubadilishana uzoefu na kujifunza mbinu mpya za kufanya kilimo cha kisasa.

Mradi wa FO4ACP ni wa miaka mitano (2019-2023) unafadhiliwa na Shirikisho la Wakulma Kusini mwa Afrika (SACAU). Mpaka sasa mradi umefanikiwa kuwafikia wakulima wadogo wapatao 19,000 wakiwemo wanawake na vijana katika Wilaya ya Mvomero (Mkindo na Dakawa), inakadiriwa mpaka Desemba2023 wakulima 24000 watanufaika na mradi.



# WAKULIMA NA WAUZA PEMBEJEO WAJADILI

Mei 10 na 11 2023, ACT iliendesha warsha ya siku mbili iliyohusu ***"Mahusiano ya kibiashara"*** kwa wakulima wa wilaya ya Mvomero, Mkoani Morogoro kutoka skimu ya umwagiliaji za Mkindo na Dakawa. Warsha hiyo ililenga kuboresha mahusiano ya kibiashara baina ya wauzaji wa pembejeo na wakulima. Jumla ya washiriki 74 walihudhuria mjadala huo ikijumuisha wakulima viongozi 62, wakala wa pembejeo 6 na maafisa ugani 6 wote kutoka Mkindo na Dakawa. Katika mkuatno huu, majadiliano yalijikita zaidi katika bei ya bidhaa, taraibu za malipo, ubora wa bidhaa na masuala mengine yanayolenga kuboresha mazingira ya kibiashara.

Pia washiriki waliaanisha changamoto wanazokabiliana nazo tangia mfumo wa ruzuku uanzishwe kama vile upatikanaji wa bidhaa kwa wakati, mitaji na bei n.k  Warsha hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa mradi wa FO4ACP (2019-2023) unaofadhiliwa na Shirikisho la Wakulima Kusini mwa Afrika (SACAU) unaolengo kuongeza pato la mkulima. Warsha iliendeshwa na  Bw. Obed Abraham, Bw. Khalid Ngassa kutoka Sekretarieti ya ACT, na Bw. Hoziel Foya - mwakilishi wa ACT Mvomero.



ACT
Agricultural Council of Tanzania

**Mahali**
Plot 88 C, block 45, House no. 3. Off Bagamoyo Road Victoria

**Namba ya Simu**
(+255) 719260726

**Tovuti**
www.actanzania.or.tz

## Dira na Dhamira

### MISSION

Kuwa na sekta ya kilimo iliofanikiwa, endelevu na shindani inayohakikisha usalama wa chakula na lishe unaotokana na

### VISION

Kutetea, kuratibu na kuwezesha mazingira rafiki kwa kilimo-biashara

## Bodi ya Uhariri

- Bw. Timoth Mmbaga – Mwenyekiti
- Bw. Mark Magila - Mjumbe
- Bw. Khalid Ngassa - Mjumbe

## Wasiliana Na.

Mkurugenzi Mtendaji
Agricultural Council of Tanzania
S.L.P 14130, Dar es Salaam

Simu: (+255) 719260726
Barua pepe: act@actanzania.or.tz
Tovuti: www.actanzania.or.tz

## Malengo ya ACT

- Kujenga mazingira wezeshi kwa kilimo-biashara
- Kujengea uwezo wanachama wa ACT katika utoaji wa huduma
- Kutuma na kupokea taarifa kutoka kwa wanachama na wadau wengine zinazohusu ustawi wa sekta ya kilimo nchini
- Kuratibu na kuendesha mashirikiano katika ngazi ya taifa na wilaya
- Kuratibu jitihada za sekta ya umma na binafsi katika uenddelezaji wa kilimo-biashara

## Hii Ndiyo PFS

Ubia wa mradi wa PFS unaratibu na kuwezesha watendaji mbalimbali kwenye mnyororo wa thamani wa wadau chini ya mfumo wa mashirikiano kati ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Mradi unatekelezwa na Baraza la Kilimo Tanzania. Lengo lake ni kuchangia na kuongeza kiwango cha mafanikio yaliyopatikana kwenye awamu ya pili ya Mradi wa Ubia wa Kilimo Tanzania (TAP2) katika kipindi cha Oktoba 2014 hadi Mei 2020. Mradi huo ulifanikiwa ukuaji wa kilimo kwa kutumia mbinu za kilimo-biashara na uwekezaji.

### Malengo ya Mradi

Lengo kuu ni; Kuongeza usalama wa chakula na lishe, nakupunguza umasikini. Umaskini unatarajiwa kupungua kwa 17%, halikadhalika na ukosefu walishe kwa Watoto kupungua kwa 5%.

### Utaratibu wa utekelezaji

Mradi utatumia mbinu ya ubia katika utekelezaji wa mradi. Mradi wa PFS, chini ya Baraza la kilimo Tanzania (ACT). Utaratibu na kuongeza uwezeshaji na utekelezaji ili kuhakikisha ubia unahimarishwa na mafanikio tarajiwa yanafanikiwa. Mradi unatumia ujuzi na maarifa ili kutatua vikwazo muhimu kwenye mnyororo wa thamani. Mradi umeainisha asasi za kiraia 35, wabia kutoka sekta ya umma na binafsi (ndani na nje ya nchi), wenye uwezo na majukumu mbalimbali watakao shirikishwa katika kazi ya ubia.

### Akaunti za Mitandao ya Kijamii:

LinkedIn @barazalakilimo
Twitter @act_tz
Instagram barazalakilimotanzania
Facebook Agricultural Council of Tanzania

**PFS inawajibika kwa Bodi ya Wakurugenziwa ACT**